FACES OF THE PANDEMIC

Hadi wa leo karibu watu milioni arubaini wana ishi na ugonjwa wa ukimwi duniani**.** Tayari watu milioni ishirini na tano wame aga dunia kutokana na ugonjwa huu au kutokana na maradhi yanaoletwa na ugonjwa huu**.** Kwa kweli ugonjwa huu umeadhiri watu wengi duniani **.**ukimwi inapatikana nchi zote duniani lakini kuna nchi zingine ambazo zimeadhiriwa zaidi.Afrika ndiyo bara ambayo imeadhiriwa vibaya na ugonjwa huu.

Ukimwi una adhiri kila mtu kwenye familia ,wamama waja wazito wenye virusi wana weza pitisha virusi hizo kwa watoto wao ambao hawajazaliwa ,wazazi wanaaga dunia na kuwawacha watoto wao wakiwa yatima na pesa nyingi pia zinatumika kwenye matibabu ya kila siku. Afrika ina yatima karibu milioni kumi na nne kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi. Ugonjwa huu umeadhiri kila mtu ,yule ambaye ana virusi pamoja na yule ambaye hana virusi. Ugonjwa huu una husu dunia nzima, makabila mbali mbali pamoja na familia. Milioni ya mayatima wana kuwa wakubwa bila kujua njia za kujitegemea ,hawana mitaji ya kutosha na wana dharauliwa na jamii. Ni lazima tutafute njia za kumaliza ukimwi duniani haijalishi kama wewe ni maskini, mwalimu, waziri au tajiri ni muhimu tuungane pamoja kutafuta njia za kumaliza ugonjwa huu wa ukimwi.

Africa Kusini:

Afrika kusini ina watu zaidi ya milioni arubaini na iko na uchumi imara Afrika. Wanaume wanatazamiwa kuishi miaka arubaini na saba(47) na wanawake miaka arubaini na tisa(49) na asilimia thalathini na nne(34%) ya wananchi wana ishi chini ya dola mbili kwa siku. Zaidi ya watu milioni tano na nusu wanaishi na ugonjwa wa ukimwi na kati ya hawa, watu wazima ni asilimia kumi na nane na nukta nane(18.8%) yaani kwa kila watu watano mmoja wao ana virusi vya ukimwi. Mpaka wa leo watoto milioni mmoja na laki mbili ni mayatima kwasababu ya ugonjwa huu na kwa watoto hawa laki mbili na elfu arubaini (240,000) wana virusi vya ukimwi.

Swaziland:

Swaziland imeadhiriwa kushinda afrika kusini lakini asilimia ya watu wenye ugonjwa huu uko chini kwani ni nchi ndogo (watu milioni moja). Wanawake wanatarajiwa kuishi miaka thelathini na tisa(39) na wanaume thelathini na sita(36). Ina kisiwa watu laki mbili na elfu ishirini wanaishi na ugonjwa wa ukimwi yaani asilimia thelathini na tatu nukta nne(34.4%) ya wananchi kati ya miaka kumi na mitano mpaka arubaini na tisa (15 - 49) Na ni asilimia kumi na moja (11%) tu ya wamama wajawazito wanaopata matibabu ya kuzuia virusi ku wapata wanao ambao bado hawajazaliwa.

Ethiopia:

Ethiopia ni moja ya nchi Afrika ambayo ina watu wengi, zaidi ya milioni sabini na saba, lakini wako na asilimia ya chini ya ugonjwa wa ukimwi kuliko afrika kusini na swaziland. kwa sasa asilimia ya ugonjwa huu haujulikani kwa uhakika na unawekwa asilimia nne(4%) kutoka asilimia nukta tisa hadi asilimia tatu na nusu (0.9- 3.5%) kulingana na UNAIDS. Asilimia themanini (80%) ya wa Ethiopia wanaishi chini ya dola mbili kwa siku , na watu wanatarajiwa kuishi hadi miaka hamsini. UNAIDS haina uhakika watu wangapi wana virusi vya ukimwi na umewekwa kati ya watu nusu milioni hadi milioni moja na laki tatu (serikali imeweka watu wenye virusi kuwa milioni moja na laki sita). Mayatima wa ugonjwa huu ni karibu laki tisa ,na asilimia ishirini na tano(25%) pekee ndio wanao enda shule. Chini ya asilimia moja ya wamama waja wazito wenye virusi hawapati matibabu ya kuzuia virusi kuwapata wanao.

Nigeria:

Nchi ya nigeria ni kama Ethiopia, ukimwi una adhiri asilimia nne(4%) ya wananchi ambao ni zaidi ya milioni mia moja na thelathini na tatu na hii inafanya nchi ya nigeria kuwa na watu zaidi walio na virusi vya ukimwi duniani. Watu wanatarajiwa kuishi hadi miaka arubaini ,na zaidi ya asilimia tisaini(90%) wanaishi chini ya dola mbili. Kulingana na UNAIDS karibu watu milioni tatu wana virusi vya ukimwi Nigeria na wale wameaga dunia wamewacha karibu yatima milioni moja. Chini ya asilimia moja(1%) ya wanawake waja wazito wanapata matibabu ya kukinga wanao na ni asilimia kumi na nane(18%) pekee wameenda shule na wanajua njia za kujinga kutokana na ukimwi.

India:

India iko na watu zaidi ya bilioni moja na ukimwi ina adhiri watu karibu asilimia moja(1%) yaani karibu watu milioni sita wanaishi na virusi vya ukimwi. Watu wanatarajiwa kuishi hadi miaka sitini na zaidi ya asilimia themanini(80%) ya watu wanaishi chini ya dola mbili kwa siku.Wanaopata matibabu ni asilimia saba(7%) pekee na wamama wajawawazito wanaopata matibabu ya kuzuia kueneza virusi kwa watoto ni asilimia moja nukta sita(1.6%) tu.Watu wanatumia kondomu kwa wingi na pia watu wengi wamefikiwa na kufundishwa juu ya ugonjwa huu wa ukimwi.

Amerika:

Karibu watu milioni mia tatu wanaishi Amerika na walio adhiriwa na ukimwi ni chini ya asilimia moja(1%).Kati ya watu milioni moja na laki mbili wana virusi na asilimia sabini(70%)wanapata matibabu.

Ukraine:

Nchi hii ambayo iko uropa magharibi iko na watu milioni arobaini na sita na walio na virusi ni asilimia moja nukta nne(1.4%). Zaidi ya watu laki nne wanaishi na virusi na nambari hii inaendelea kuongezeka. Asailimia thelathini(30%) ya wamama waja wazito wana pokea matibabu na watu wengi wanatumia kondomu. Asilimia saba(7%) tu ya wale wanao virusi ndio wana pata matibabu.

Thailand:

Thailand iko na wananchi karibu milioni sitini na tano , na asilimia thelathini na mbili(32%) wanaishi chini ya dola mbili.Zaidi ya watu nusu milioni wanaishi na virusi vya ukimwi yaani asilimia moja na nukta nne(1.4%) ya watu wazima. Asilimia thelathini(30%) ya wamama waja wazito wana pata matibabu ya kuzuia kupitishia wanao virusi na asilimia sitini(60%) ya wale walio na virusi wanapata matibabu.

Brazil:

Nchi hii iko na zaidi ya watu milioni mia moja na themanini na tano na walio na virusi ni chini ya asilimia moja (0.5%). Wananchi wana tarajiwa kuishi hadi miaka sabini , na asilimia ishirini na mbili (22%) ya watu wanaishi chini ya dola mbili kwa siku. Karibu watu laki sita na elfu ishirini wanaishi na virusi vya ukimwi na karibu ya asilimia sitini(60%) ya wamama waja wazito wanapata matibabu ya kuzuia kueneza virusi kwa wanao.

Uganda:

Uganda ina wananchi milioni ishirini na tisa na kati ya hawa asilimia saba (7%)wana virusi vya ukimwi yaani watu milioni moja, watoto mayatima ni karibu milioni moja na kati ya hawa laki moja wana virusi vya ukimwi. Watu wanatarajiwa kuishi hadi miaka hamsini. Asilimia kumi na mbili(12%) ya wamama waja wazito wapata matibabu na zaidi ya watu aslimia hamsini(50%) wana pata matibabu kulingana na UNAIDS. Utumiaji wa kondomu ni karibu asilimia hamsini(50%) na wanaume bado wana fanya mapenzi na zaidi ya mpenzi mmoja.

Swali : kwanini ukimwi ni ugonjwa muhimu kwetu sote na ni lazima tuhusike?

Kutoka ugonjwa huu wa ukimwi ujulikane makosa mengu yametendeka na ni lazima tusome kutokana na makosa hayo. Hakuna tiba la ukimwi na kwa hivyo masomo juu ya njia za kujikinga ni jambo la maana kwani inatufundisha njia za kujikinga. Bado ugonjwa huu haujulikani vizuri na maswali yote hayawezi kujibiwa lakini bado uchunguzi unaendelea kufanywa.

Tayari tumeongea juu ya vile ukimwi una adhiri uchumi ,na vile una hisi ni muhimu sana katika hii jamii ? ni madhara gani yanaletwa na ugonjwa huu ?

Maoni :

1. ukosefu wa kazi
2. Mayatima
3. Watu kuishi maisha mafupi ,kuongezeka kwa ugonjwa kama T.B na matibabu ya hali ya chini kwani hospitali zote zimejaa watu wanao adhirika na ugonjwa huu.
4. Kutopata kazi kwa wale ambao ni wagonjwa pamoja na wale wanao wachunga
5. Matibabu ghali .ukosefu wa chakula, kutokuwa na njia za kujisaidia ,kukosa masomo ,watotot kufanya kazi na vifo
6. Kudharauliwa na jamaa na jamii.
7. Kutokua na habari ya kutosha juu ya ugonjwa huu .
8. Watu wa nchi wenye nguvu na wanao fanya kazi wanaadhiriwa na ugonjwa huu na kusababisha kuzoroteka kwa uchumi.
9. Mahitaji yote ya nchi yanawekwa kando ili kutumia mitaji yote kukinga ukimwi.

Kumekuwa na mafanikio pamoja na makosa katika kutafuta matibabu ya ukimwi. Utengenezaji wa matibabu ume weza kudumisha maisha ya mamilioni ya watu duniani. Ingawaji matibabu haitibu ugonjwa ,lakini inasaidia watu wenye virusi .matibabu hii inatumika kwa muda mrefu na ni ngumu saa zingine kufuata maagizo na pia zingine zinadhuru afya. Shida kubwa zaidi ni kupata njia ya kupelekea walio na virusi madawa haya.

Wakati matibabu yalipatikana makampuni mengi yalikataa madawa yao kutengenezwe na kampuni zingine , hii amri inakubaliwa kimataifa na inaitwa TRIPS (Trade-Related Intellectual Property Rights). Na kwa sababu hii madawa haya yalikuwa ghali, karibu dola elfu kumi kwa mwaka. Majadiliano kati ya jumuiya za kimataifa na serikali ya Amerika yalifanywa na serikali ya Brazil na watu wanaoishi na virusi vya ukimwi pamoja na jumuiya za kibinafsi.

Brazil:

Kipimo cha kwanza halisi Brazil kilifanywa mwaka wa elfu moja mia tisa na themanini(1980) na kwasababu ya hii jumuiya ndogo ndogo zikaanzishwa. Kanisa ya katholiki ili shinikiza serikali kufundisha watu juu ya ugonjwa huu ili kuanzisha mabadiliko. Serikali iliweza kufanya kondomu rahisi na kuweza kueneza milioni ya kondomu bure ,hii iliweza kupandisha utumiaji wa kondomu kutoka asilimia nne hadi asilimia arubaini na nane (4% - 48%) mwakani elfu moja mia tisa tisini na tisa(1999). Matibabu yaliendelea kutengenezwa na serikali ili waweza kufanya matibabu bure kwa mwananchi yeyote mwenye virusi vya ukimwi. Ili kuweza kupati wanannchi matibabu ya bure serikali ya brazil ili vunja amri na kuanza kutengeneza madawa na vifo vya walioadhiriwa na ukimwi ukashuka hadi asilimia hamsini na nne.

Brazil iliungwa mkono na makampuni kubwa ambao wali omba jumuiya ya kimataifa World TradeOrganization na serikali ya marekani kuwacha kutengeneza madawa haya. Brazil ilipata njia ya kutengeneza madawa bila kuvunja amri yoyote na ika weza kutengeneza madawa hayo.Makampuni ya madawa yalijitetea na kusema ya kwamba kutengeneza madawa haya ilikuwa ni garama kubwa.

Jumuiya ya kibinafsi Doctors Without Borders ina himiza mataifa kuanza kutengeneza madawa lakini bado haijafaulu. Brazil ime toa fursa kwa mataifa zingine kwa kukubali kuwapatia na kuwafundisha njia za kutengeneza madawa.

Afrika Kusini:

Kwa kulinganisha brazil na nchi zingine ,tunaweza kuangalia Afrika kusini nchi ambayo ina makampuni mengi ya kutengeneza madawa. Pia nchi hii ndio nchi ambayo iko na uchumi imara Afrika ,wakati wa mandela ukimwi ulikuwa asilimia nane(8%). Rais mbeki alipoingia bado mabaliko hayakufanywa na mwaka wa elfu mbili na moja(2001) ukimwi ulifika asilimia ishirini(20%) ,kwa sababu hii Mbeki alimtafuta daktari mmoja kutoka marekani ambaye alisema virusi yaani HIV hayakuleta ugonjwa wa ukimwi yaani AIDS. Msimamo huu haukufurahisha watu na mwaka wa elfu mbili madaktari elfu tano walikutana Durban, Afrika Kusini na kukubaliana yakuwa virusi vya HIV ndio vinasababisha ukimwi. Serikali ya Afrika Kusini ilipelekwa kotini na watu wanao ishi na ukimwi na jumuiya za kibinafsi na wakashindwa. Na serikali ikaanza kutoa matibabu ya bure ili kuzuia upitishaji wa virusi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto wake.Kwa hivyo tunaona vile seriakli inaweza kusaidia au kudhuru wananchi wake.